PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY

Efficient and Fair Appeals Dispensation

PPAA

MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

PPAA

Toleo Na: 05 Aprili - Juni 2025

# BULLETIN

UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## MAPINDUZI MAKUBWA SEKTA YA UNUNUZI WA UMMA NCHINI:

## Wazabuni 873, taasisi 500 wafikiwa mafunzo ya moduli

MPENDWA msomaji wa Jarida hili la "PPAA Bulletin" karibu tena ujisomee toleo la tano (05) la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA). Jarida hili hutumika kama njia mojawapo ya Mawasiliano ya Kimkakati ya PPAA katika kuuhabarisha umma kuhusu majukumu na shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi mitatu. Jarida hili ni muendelezo wa majarida mengine yaliyopita yanayokuhabarisha kuhusu shughuli za PPAA kwa kipindi cha miezi mitatu.

Ninayo furaha kukuletea toleo la tano la PPAA Bulletin kwa kipindi kingine tena cha Aprili – Juni, 2025, kwa lengo la kukuhabarisha juu ya shughuli mbalimbali zilizotekelezwa kwa kipindi tajwa hususan Makala Maalumu ya mafanikio ya idara na vitengo vya PPAA ili kuweka mawasiliano ya karibu na wadau wa sekta ya ununuzi na umma kwa ujumla.

Mbali na kutekeleza jukumu lake la msingi la kushughulikia malalamiko na rufaa zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi tajwa, PPAA imefanikiwa kutoa elimu kwa wazabuni 873 na wakuu wa idara/vitengo vya ununuzi na sheria wapatao 1,588 kutoka katika taasisi nunuzi 500.

Mafunzo hayo yametolewa katika kanda mbalimbali ambazo ni Kanda ya Pwani, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati.

Aidha, katika toleo hili, tumekuandalia habari mbalimbali za kuuhabarisha umma utekelezaji wa majukumu ya PPAA katika kufikia malengo iliyokusudia kwa kipindi tajwa.

Karibu usome jarida hili ili ufahamu kwa undani PPAA na shughuli mbalimbali ilizozitekeleza katika kipindi cha miezi mitatu (Aprili – Juni, 2025) na kuendeleza ushirikiano imara katika utoaji rufaa kwa ufanisi, kwa wakati na kwa haki kwenye sekta ya ununuzi wa umma nchini.

***#Kazi Iendelee.***

# PPAA yaainisha mafanikio yake chini ya Serikali ya Awamu ya Sita

**TANGU Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilipoingia madarakani Machi 19, 2021 imekuwa ikidumisha misingi ya utawala bora hususan haki na usawa.**

**Kutokana na misingi hiyo, Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na mambo mengine, imeendelea kusimamia miradi ya kimkakati yenye tija kwa nchi na hivyo kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa umma.**

**Kwa mantiki hiyo, makala ya leo itaangazia zaidi Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ikiwa ni taasisi inayojitegemea chini ya Wizara ya Fedha iliyoundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 112 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya mwaka 2023.**

**Katika kipindi cha uongozi wa Rais Dkt. Samia, PPAA imeendelea kutekeleza jukumu lake kuu la utatuzi wa migogoro itokanayo na michakato ya ununuzi wa umma kwa haki, uwazi, uadilifu na kwa muda mfupi ili kuwezesha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha na kufikia malengo ya kutoa huduma bora kwa wananchi kwa wakati.**

**PPAA ikiwa ni moja kati ya taasisi zinazosimamia masuala ya haki katika sekta ya ununuzi wa umma inakuletea mafaniko yake kwa vitengo na sehemu zake ambazo ni Kitengo cha Usimamizi wa Rufaa za Manunuzi na Huduma za Sheria, Kitengo cha Huduma za Taasisi, Sehemu ya Usimamizi wa Rufaa, Sehemu ya Huduma za Sheria, Sehemu ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Sehemu ya Uhasibu na Fedha, Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma na Sehemu ya Ufuatiliaji Mipango na Tathmini.**




**BODI YA UHARIRI**

**Mwenyekiti**
Florida Mapunda

**Mhariri**
Gloria Tesha
Mwandishi wa TSN

**Wajumbe**
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga

**Katibu**
Nelson Kessy

**Mawasiliano:**
**Katibu Mtendaji**
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz

# Kitengo cha Usimamizi wa Rufaa za Manunuzi na Huduma za Sheria



***Bi. Florida Mapunda,** Meneja wa Idara ya Usimamizi wa Rufaa na Huduma za Sheria*

PPAA kupitia Idara ya Usimamizi wa Rufaa na Huduma za Sheria ina jukumu la kusimamia na kushughulikia rufaa zote zitokanazo na michakato ya ununuzi wa Umma. Mamlaka husimamia utawala bora kupitia utatuzi wa migogoro inayowasilishwa mbele yake kwa kuhakikisha kuwa zabuni zinatolewa kwa wazabuni wenye sifa stahiki za kufanya kazi husika na hivyo kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa umma.

Bi Mapunda anasema PPAA kwa kipindi cha miaka minne imetekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo kushughulikia rufaa, kushiriki kutengeneza Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 na Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2025; kutoa mafunzo kwa taasisi nunuzi na wazabuni na kushiriki katika maonesho na makongamano mbalimbali kwa lengo la kutoa elimu kwa umma.

"Katika idara ninayoisimamia imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni Sehemu ya Rufaa na Sehemu ya Huduma za Sheria," anaeleza Bi Mapunda.

## A) Sehemu ya Usimamizi wa Rufaa



**Bi. Violet Limilabo,** ***Mkuu wa Sehemu ya Rufaa***

Katika kipindi cha miaka minne PPAA kupitia Sehemu ya Rufaa imefanikiwa kusajili mashauri takriban 171 yaliyotokana na michakato ya ununuzi wa umma. Aidha, katika mashauri hayo, PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa zabuni 37 kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika. Hatua hiyo iliepusha utekelezaji usioridhisha wa miradi unaosababisha upotevu wa fedha za umma na kuchelewesha maendeleo stahiki kwa wananchi.

Serikali ya Awamu ya Sita inaamini usuluhishi wa migogoro hauwezi kupatikana penye ubaguzi na pale ambapo kuna wanaokosa fursa na haki zao za kiuchumi na kiraia. Hivyo, kitendo cha PPAA kuzuia utoaji wa tuzo kwa wazabuni 37 waliokosa sifa kinaweka uzito katika usuluhishi wa migogoro ambayo ni moja kati ya falsafa za Rais Dkt. Samia.

PPAA imeendelea pia kudhibiti taasisi nunuzi kukiuka taratibu za kisheria hasa katika kufanya tathimini ya zabuni (tender evaluation); katika baadhi ya mashauri, PPAA ilifanikiwa kubaini ukiukwaji wa taratibu za kufanya tathimini uliofanywa na taasisi nunuzi ikiwemo kutokuzingatia vigezo vilivyowekwa katika kabrasha la zabuni au kuongeza vigezo vipya ambavyo havikuwepo awali.

### B) Sehemu ya Huduma za Sheria

***Bi. Agnes Sayi, Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria***



PPAA kwa kipindi cha miaka minne imetekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo kushiriki kutengeneza Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 na Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2025; kutoa mafunzo kwa taasisi nunuzi na wazabuni pamoja na kushiriki katika maonesho na makongamano mbalimbali ili kutoa elimu kwa umma ambapo PPAA imeshiriki katika kutungwa upya kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 na Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2025. Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma imeleta maboresho mbalimbali katika eneo la ununuzi na ugavi ikiwemo kupunguza muda wa kushughulikia malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

Kadhalika, muda wa kuwasilisha malalamiko kwa taasisi nunuzi umepunguzwa kutoka siku saba (7) za kazi hadi siku tano (5) za kazi. Kadhalika, muda wa Afisa Masuuli wa kushughulikia malalamiko ya zabuni umepunguzwa kutoka siku saba (7) za kazi hadi siku tano (5) za kazi. Aidha, pale ambapo Afisa Masuuli ataunda jopo la mapitio ya malalamiko basi atatakiwa kutoa uamuzi wake ndani ya siku saba (7) za kazi na atatakiwa kuwajulisha wazabuni wote walioshiriki katika zabuni inayolalamikiwa ndani ya siku moja kuwa ameunda jopo la kupitia malalamiko husika. Pia muda wa kuwasilisha rufaa PPAA umepunguzwa kutoka siku saba (7) za kazi hadi siku tano (5) za kazi; na muda wa PPAA kushughulikia malalamiko au rufaa umepunguzwa kutoka siku arobaini na tano (45) hadi siku arobaini (40).

Kutokana na mabadiliko yaliyoletwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 pamoja na kanuni zake, PPAA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini, imeandaa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2025 zilizotangazwa kwenye Gazeti la Serikali tarehe 31/01/2025 kupitia GN No.65/2025. Moja kati ya maboresho yaliyoletwa na kanuni yanaendana na matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 ni takwa la kuwasilisha malalamiko na rufaa kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST).

PPAA imefanikiwa kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kieletroniki katika kanda mbalimbali ambapo mpaka sasa Kanda ya Pwani, ya Ziwa, Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati zimepatiwa mafunzo. Aidha, katika mafunzo haya PPAA imefanikiwa kutoa elimu kwa wazabuni 873 na wakuu wa idara/vitengo vya ununuzi na sheria wapatao 1,588 kutoka katika taasisi nunuzi 500.

Pia, PPAA imefanikiwa kushiriki katika maonesho na makongamano mbalimbali yakiwemo Sabasaba, Nanenane, Kongamano la Ununuzi wa Umma la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPPF), Kongamano ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi, Wiki ya Sheria, Maonesho ya Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) pamoja na Kongamano la Tisa la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2025. Katika maonesho na makongamano hayo, PPAA ilifanikiwa kutoa elimu kuhusu majukumu yake pamoja na matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kieletroniki.

## Kitengo cha Huduma za Taasisi



***Bw. Paschal Kajuna, Meneja wa Huduma za Taasisi***

Kitengo cha Huduma za Taasisi kinajukumu la kuhakikisha utendaji na ufanisi katika utawala, usimamizi wa rasilimaliwatu na fedha. Katika kipindi cha miaka minne (4) kimehakikisha masuala yanayohusu utawala, usimamizi wa rasilimali watu na fedha yanafanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na serikali ili kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya mamlaka.

Kwa upande wa utawala na usimamizi wa rasilimaliwatu tumehakikisha masuala yote yanayohusu usimamizi wa utendaji kazi, mafunzo kwa watumishi, nidhamu, mishahara na ustawi wa watumishi yanafanyika kwa ukamilifu. Aidha katika usimamizi wa fedha, tumehakikisha uwazi, uwajibikaji na uendelevu wa kifedha katika mamlaka, hii ni pamoja na kuhakikisha usimamizi thabiti wa bajeti, uhasibu na utunzaji wa hesabu, ili kuhakikisha fedha za umma zinasimamiwa kwa ufanisi na uwajibikaji na kuwezesha PPAA kufikia mipango yake ya kimkakati.



Sehemu ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu inasimamiwa na **Bw. Mohamed Makame** ambapo katika kipindi cha miaka minne imefanikiwa katika nyanja zifuatazo:

**a) Maadili na nidhamu kwa watumishi**

PPAA imefanikiwa kuendeleza usimamizi mzuri wa maadili ya utumishi wa umma na nidhamu ya kazi kwa watumishi wake. Katika kipindi cha miaka minne hapakuwa na mtumishi aliyekuwa na shauri la kinidhamu. Hii inatokana na watumishi kujengewa uelewa kuhusu maadili na taratibu zinazosimamia utumishi wa umma na hivyo kuepuka migogoro na makosa ya kimaadili na nidhamu.

**b) Muundo wa Taasisi (Organisation structure)**

Muundo wa PPAA umeboreshwa kutoka muundo wa zamani wa mwaka 2007 uliokuwa na mapungufu yaliosababisha changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi. Kwa sasa muundo wa mamlaka ulioidhinishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili 2024 umegawanyika katika vitengo na sehemu tofauti na wa awali ambao haukuwa na vitengo wala sehemu.

**c) Muundo wa Maendeleo ya Utumishi (Schemes of Services)**

Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa PPAA umeboreshwa kutoka muundo wa mwaka 2007 uliokuwa na mapungufu yaliosababisha changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya

taasisi. Miongoni mwa mapungufu ya muundo wa zamani ni pamoja na kutokuwapo kwa majukumu na nafasi za wakuu wa vitengo au sehemu, kutokutambua baadhi ya taaluma kama mipango, uhusiano kwa umma, mwandishi, mwendesha ofisi n.k. Muundo mpya ulioidhinishwa Oktoba, 2024 umerekebisha mapungufu hayo.

**d) Matumizi ya mifumo ya kielektroniki**

PPAA inatumia mifumo iliyotambulishwa na serikali kutoa huduma ndani na nje ya taasisi mfano matumizi ya mfumo wa MUSE, GePG, PlanRep, e-Watumishi, Watumishi Portal, e-Office, Government mail, e-Board, e-Mrejesho, e-Vibali, Staff Assessment, GAMIS, Digital Signature, NeST, na katika utekelezaji wa jukumu kuu la PPAA la usuluhishi wa migogoro itokanayo na michakato ya zabuni, uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa zote unafanyika kupitia *(Complaints and Appeal Management Module)* ndani ya NeST.

**e) Kuboresha afya za watumishi**

Mamlaka imeendelea kulinda nguvu kazi ya taifa kwa kusimamia uimarishaji wa afya za watumishi wake kupitia utoaji wa elimu ya afya ikiwemo lishe bora, elimu ya Ukimwi, magonjwa sugu yasiyoambukiza na elimu ya afya ya akili. Mamlaka pia imetoa fursa kwa watumishi wake kushiriki michezo kwa kununua vifaa vya kufanyia mazoezi ambapo watumishi hushiriki mazoezi kwa pamoja ikiwemo pia kuhudhuria matukio ya michezo yanayoandaliwa na wizara au taasisi nyingine.

## Kitengo cha Fedha na Uhasibu



***Bw. Aliko Mwaiteleke,***
***Mkuu wa Kitengo cha Fedha***

KITENGO hiki cha Fedha na Uhasibu kinachosimamiwa na Bw. Aliko Mwaiteleke kimefanikiwa kuongeza mapato kwa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA). Kimechangia mamlaka kujenga Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kieletroniki katika Mfumo wa NeST.

Vilevile, PPAA kwa kipindi cha miaka minne kupitia Kitengo cha Fedha na Uhasibu imefanikiwa kutekeleza jukumu la ulipaji wa fedha kwa kuzingatia taratibu na miongozo iliyopo.

Aidha, kimehakikisha watu wanafuata sheria na taratibu za fedha kwa makundi mbalimbali ikiwemo stahili za watumishi na watoa huduma mbalimbali zilizotokana na mikataba kama ulinzi, usafi, huduma za intaneti, simu, umeme na kadhalika. Hivyo kitengo kimesaidia kupunguza hoja za wakaguzi wa nje na ndani.

Pia katika kipindi cha Miaka minne ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Kitengo cha Fedha na Uhasibu kimepatiwa hati safi kwenye kaguzi zote zilizofanyika. Kupitia hati hizo safi, Mamlaka ya Rufani imedhihirisha kuwa na usimamizi mzuri wa rasilimali Fedha.

## Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma



***Bw. Nelson Kessy,***
***Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma***

Katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, kitengo hiki pamoja na mambo mengine kimeendelea kuwa daraja muhimu kuhakikisha taarifa na shughuli ambazo PPAA inashiriki zinaufikia umma kwa wakati kupitia vyombo vya habari nchini. Aidha, PPAA kupitia Kitengo cha Uhusiano na Mawassiliano kwa Umma imefanikiwa katika mambo yafuatayo:-

**a) Kuandaa Mkakati wa Mawasiliano wa Mamlaka:**

PPAA kupitia Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma imefanikiwa kuandaa Mkakati wa Mawasiliano (Communications Strategy), ambao umeainisha mbinu za kimkakati zinazolenga kuwezesha mamlaka kuwasiliana na wadau wake kama taasisi nunuzi, wazabuni, vyombo vya habari, wajumbe wa mamlaka ya rufani na kadhalika.

Mkakati huo wa mawasiliano umesaidia kufanikisha dhana ya mawasiliano ya kimkakati baina ya taasisi, wafanyakazi na wadau wake kuhusu shughuli zake na kupata matokeo yake.

Kadhalika, mkakati wa mawasiliano umesaidia kuweka mawasiliano thabiti na yenye tija bora kutoka kwa watumishi kwenda kwa wadau; pia umesaidia kuanzisha chapa (brand) sahihi, ambayo ni njia rahisi ya kuwasilisha ujumbe wa PPAA kwa wadau wake kwa wakati uliokusudiwa.



**b) Kuanzisha na kuhuisha mitandao ya Kijamii**

Kutokana na kukua kwa Sayansi na Teknolojia, nguvu ya mitandao ya kijamii imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa katika kupashana habari nchini na duniani kwa ujumla.

Matumizi ya mitandao ya kijamii kama vile facebook, twitter, WhatsApp, You Tube na Instagram kwa sasa ndiyo njia rahisi ya kusambaza taarifa au ujumbe wa kuwafikia watu wengi zaidi kwa muda mfupi. Aidha, PPAA imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutumia mitandao ya kijamii ya Facebook, Instagram, X (Twitter) na You Tube kuwasiliana na wadau wake, kuchapisha taarifa zake na kutoa taarifa za matukio inayoyatekeleza kwa wakati husika.

Kupitia mitandao ya kijamii, PPAA imefanikiwa kukuza utambulisho wake na kuongeza thamani yake kwa wadau wa ununuzi wa umma na kuendelea kutoa huduma bora kwa weledi wa hali ya juu zaidi.

**c) Kuandaa Jarida la Mtandaoni la PPAA Bulletin**

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma kimeanzisha Jarida la PPAA Bulletin ambapo jarida hilo hutumika kama njia mojawapo ya mawasiliano ya kimkakati ya mamlaka kuhabarisha wadau wa ununuzi wa umma na umma kwa ujumla kuhusu majukumu na shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi mitatu.




Jarida hilo limekuwa likijumuisha shughuli ambazo hutekelezwa na PPAA kwa kipindi cha miezi mitatu ya kila robo ya mwaka wa fedha (Quartely). PPAA imefanikiwa kuchapisha matoleo matano ya Bulletin na imekuwa ikisambazwa kupitia mitandao ya kijamii ya mamlaka, tovuti na mitandao mbalimbali ya kijamii hususan makundi mbalimbali ya WhatsApp ili kufikia wadau na umma wa Watanzania kwa ujumla.

# Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)



***Bw. Humphrey Kisanga,***
***Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Tehama***

**PPAA kupitia Kitengo cha Tehama imefanikiwa katika:-**

**a) Kukamilika kwa Ujenzi na Kuanza kwa Matumizi ya Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa**

Katika kutekeleza azma ya serikali ya kuimarisha uwazi, uwajibikaji, na ufanisi wa sekta ya ununuzi wa umma kushughulikia malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma, PPAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), ilikamilisha ujenzi wa Moduli ya Usimamizi wa Malalamiko ndani ya Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa Njia ya Kielektroniki (NeST).

Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilizindua rasmi matumizi ya moduli hiyo Februari 2025. Baada ya uzinduzi huo, moduli imeleta mageuzi chanya kwa namna taasisi za umma kwa kushurikiana na PPAA zinavyopokea, kusajili na kushughulikia malalamiko na rufaa kutoka kwa wazabuni walioshiriki katika michakato ya ununuzi wa umma.

Kwa sasa, malalamiko yanawasilishwa kupitia moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa iliyopo katika mfumo wa NeST hatua inayolenga kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji, utunzaji wa kumbukumbu katika kushughulikia malalamiko na rufaa.

Aidha, Kitengo cha Tehama kimefanikiwa pia kuanzisha matumizi wa Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Vikao vya Menejimenti. Katika kuimarisha utendaji wa ndani, Kitengo cha Tehama kimeanzisha matumizi ya mfumo wa elektroniki unaowezesha kufanyika kwa vikao vya menejimenti kwa njia ya mtandao (online), hatua inayochochea ushiriki na ufanisi wa maamuzi hata kwa walioko nje ya ofisi.

**b) Matumizi ya Sahihi ya Kidijitali (Digital Signature)**

Ili kuimarisha uhalali wa nyaraka na kurahisisha mchakato wa kuidhinisha nyaraka rasmi, Kitengo cha Tehama kimeanzisha:

Matumizi ya sahihi za kidijitali kwa viongozi waandamizi katika idhini za maamuzi ambapo imesaidia kupunguza utegemezi wa karatasi, kuongeza kasi ya mchakato wa maamuzi, na kuimarisha usalama wa nyaraka.

**c) Majaribio ya Usikilizaji wa Mashauri kwa njia ya mtandao (Pilot test)**

Mamlaka ya Rufani ya Ununuzi wa Umma (PPAA) imekamilisha ufungaji wa vifaa vya Tehama vitakavyowezesha usikilizaji wa mashauri kwa njia ya mtandao (Video Conference). Hatua hii ni sehemu ya mkakati wa mamlaka wa kutumia teknolojia kuboresha utoaji wa haki kwa wakati, kwa uwazi na kwa gharama nafuu kwa wadau wote wa ununuzi wa umma.

Kupitia utekelezaji wa zoezi hilo, mamlaka itaanza kufanya majaribio (pilot test) ya utekelezaji wa usikilizaji wa mashauri kwa njia ya mtandao.

Kupitia majaribio haya, mamlaka inalenga kupanua wigo wa upatikanaji wa haki kwa njia ya kidijitali ambayo ni rafiki kwa mtumiaji na inazingatia thamani ya muda na rasilimali za wahusika wote.

Kitengo pia kimefanikiwa kufanya majaribio ya Usikilizaji wa Mashauri kwa njia ya mtandao (Pilot test);

Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imekamilisha zoezi la ufungaji wa vifaa vya Tehama vitakavyowezesha usikilizaji wa mashauri kwa njia ya mtandao. Hatua hii ni sehemu ya mkakati wa Mamlaka ya Rufani wa kutumia teknolojia kuboresha utoaji wa haki kwa wakati, kwa uwazi na gharama nafuu kwa wadau wa ununuzi wa umma.

Kupitia mfumo huo, PPAA inalenga kupanua wigo wa upatikanaji wa haki kwa njia ya kidijitali ambayo ni rafiki kwa mtumiaji na inazingatia thamani ya muda na rasilimali za wahusika wote.

Matumizi ya moduli hii yameongeza ufanisi kwa kupunguza ucheleweshaji, kurahisisha uwasilishaji wa nyaraka na kutoa taarifa kwa wakati kupitia barua pepe kwa wadau wa ununuzi wa umma. Pia, mfumo wa NeST umejengwa kwa kuzingatia usalama wa taarifa na uwazi wa mchakato wa uamuzi. Hatua hii ni sehemu ya mkakati wa kuhakikisha haki inatendeka kwa wakati, gharama nafuu, na bila usumbufu kwa wadau wa ununuzi wa umma.

## Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi



***Bw. Stanley Jackson,***
***Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi***

Kitengo cha Ununuzi wa Mamlaka ya Rufani kwa miaka minne kinajivunia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia weledi, uzalendo na kuhakikisha kinafanya ununuzi wa kimkakati kupitia mfumo wa NeST ili kuokoa fedha za umma pamoja na kupata thamani halisi ya fedha za umma.

PPAA imefanikiwa pia kuhakikisha mnyororo wa ununuzi na ugavi unatekelezwa kikamilifu kuhakikisha bidhaa na huduma zinapatikana kwa wakati kwa kuzingatia thamani halisi za fedha za umma.

Kwa kipindi cha miaka minne Kitengo cha Ununuzi wakati wote kimehakikisha maamuzi ya Afisa Masuuli pamoja na Bodi ya Zabuni yanatekelezwa kikamilifu kwa kuzingatia taratibu husika. Aidha kitengo hiki kimepanga ununuzi, shughuli za ununuzi na uondoshaji wa mali, kupendekeza na kushauri kuhusu ununuzi uliobora na wenye tija kwa mamlaka na serikali.

## Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani



***Bi. Paulina Victor,***
***Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani***

Katika kipindi cha miaka minne PPAA kupitia Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani imefanikiwa kuweka mazingira rafiki ya kufanya ukaguzi wa ndani kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni pamoja na miongozo ya serikali.

Kitengo kimefanikiwa kufatilia utekelezaji wa hoja za mkaguzi wa nje, ambapo hoja nyingi hutekelezwa kwa wakati na hivyo kuthibitisha kuwa uzingatiaji wa sheria (compliance) unajitosheleza.

Kwa miaka minne PPAA imeendelea kupata hati safi ya ukaguzi kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali hivyo kuakisi kuwa utekelezaji wa shughuli za mamlaka unafuata kanuni taratibu na miongozo iliyowekwa (compliance).

### Hitimisho

Kwa kuwa takribani asilimia 70 ya bajeti ya serikali hutumika kwa ajili ya ununuzi wa umma, sheria, kanuni na miongozo ya ununuzi wa umma inaiwezesha serikali kuendelea kuimarisha sekta ya ununuzi. PPAA kupitia Wizara ya Fedha inaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuiwezesha kufanikisha majukumu yake kwa wakati na ufanisi na kuwa sababu ya kupata mafanikio yaliyoainishwa kupitia idara na vitengo vyake. Aidha, PPAA inaahidi kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ubunifu ili kufikia azma ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi imara wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

# PPAA yawaasa wazabuni kushiriki Mafunzo ya Moduli




*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akizungumza na waandishi wa Habari pembezoni mwa Kongamano la Tisa la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2025. Kongamano hilo limefanyika mwezi Juni, 2025 Jijini Arusha.*

**Katika jitihada za kuhakikisha kuwa Serikali inapata thamani halisi ya fedha katika miradi yake, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imewaasa wazabuni kushiriki mafunzo yanayoratibiwa na Mamlaka hiyo ili kuwajengea uwezo wa kutumia Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST.**

Rai hiyo imetolewa na Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando pembezoni mwa Kongamano la Tisa la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2025 linaloendelea Jijini Arusha. “Moduli hii imejengwa ili kusaidia umma na hususan kuendana na miongozo ya Serikali ya kuzitaka taasisi za umma kutumia tehama katika kufikisha huduma zake kwa wananchi kwa wakati uliokusudiwa,” amesema Bw. Sando

Baada ya Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuzindua rasmi matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia Malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST mwezi Februari 2025, Mamlaka ya Rufani kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeendelea za zoezi la kutoa mafunzo mahususi ya matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kieletroniki katika Kanda mbalimbali nchini.

“Katika kuhakikisha wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma wanapata mafunzo ya matumizi ya moduli PPAA imeendelea na zoezi la kutoa mafunzo mahususi ya Moduli katika kanda mbalimbali ambapo hadi sasa Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zimepatiwa mafunzo hayo,” amesema Bw. Sando

Aidha, Bw. Sando ameongeza kuwa hadi sasa PPAA imefanikiwa kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya moduli hiyo kwa wazabuni 800 na wakuu wa Idara/Vitengo vya ununuzi na sheria wapatao 1,588 kutoka katika taasisi nunuzi 500.

Bw. Sando ameongeza kuwa matumizi ya moduli yana faida nyingi zikiwemo mzabuni kutolazimika kufika katika ofisi za taasisi nunuzi au za PPAA ili kuwasilisha lalamiko au rufaa yake. Kadhalika, inasaidia kupunguza gharama na muda kwa wazabuni kwani hawatalazimika kusafiri ili kuweza kuwasilisha malalamiko au rufaa zao PPAA.

“Moduli inaongeza uwazi katika mchakato wa ushughulikiwaji wa malalamiko na rufaa kwa kuwa mzabuni aliyewasilisha lalamiko au rufaa lakini pia ataweza kuona hatua mbalimbali za ushughulikiaji wa lalamiko au rufaa yake, na kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu za taarifa za malalamiko na rufaa,” amesema Bw. Sando

Kadhalika, Bw. Sando amewasihi wazabuni kutoka mkoa wa Dodoma na mikoa jirani kushiriki mafunzo mahususi kuhusu Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kieletroniki katika mfumo wa NeST yatakayofanyika katika ukumbi wa Lavenda Hall tarehe 18 Juni 2025 Jijini Dodoma.

Awali, akitembelea mabanda ya maonesho katika viwanja vya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) kabla ya kufungua rasmi Kongamano la tisa la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2025, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb.) aliipongeza PPAA kwa kuanzisha Moduli ya kupokea na kushughulikia Malalamiko na Rufaa kieletroniki.

Pamoja na mambo mengine, Dkt. Gwajima aliahidi kuwa balozi wa hiari wa kuinadi Moduli ya kupokea na kushughulikia Malalamiko na Rufaa kieletroniki kwa wadau wa ununuzi hususan Wanawake na Makundi Maalum.




*Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria za Mamlaka (PPAA), Bi. Agnes Sayi akiwasilisha mada kwa washiriki kuhusu uzoefu wa kushughulikia malalamiko na rufaa za zabuni kupitia mifumo ya kidijitali wakati wa Kongamano la Mwaka la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2025 kwa wadau wa ununuzi wa Umma nchini. Kongamano hilo limeratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) limefanyika mwezi Juni, 2025 Jijini Arusha.*

# PPAA yatoa elimu kwa wadau wa ununuzi Maonesho ya CRB

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeshiriki maonesho ya Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2025 kwa lengo la kutoa elimu wa wadau wa ununuzi hususan Makandarasi nchini.**

PPAA imetumia maonesho hayo yaliyoratibiwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) Jijini Dar es Salaam kutoa elimu ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) katika mfumo wa NeST.

Akiongea kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando wakati wa maonesho hayo, Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria za Mamlaka (PPAA), Bi. Agnes Sayi amesema pamoja na mambo mengine, amesema kuanza rasmi kwa matumizi ya moduli hiyo kuna faida nyingi hususan kuokoa muda, gharama, kupunguza mianya ya rushwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma.

"Moduli hii mpya inatoa fursa kwa wazabuni kuwasilisha malalamiko na rufaa kwa urahisi, wakati na gharama nafuu na pia itawezesha taasisi nunuzi na PPAA kushughulikia malalamiko na rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi katika moduli, hivyo kupunguza muda na gharama zinazoambatana na zoezi zima la utoaji wa haki," amesema Bi. Sayi.

Akifungua Mkutano wa Mashauriano na na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2025, Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega (Mb.) ameitaka Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), kuwachukulia hatua makandarasi wazembe wanaosababisha hasara na athari kwa Serikali na wananchi kwa kutokamilisha miradi kwa wakati.

Waziri Ulega ametoa agizo hilo Jijini Dar es Salaam Mwezi Mei, 2025 wakati akifungua Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2025 uliobebwa na kauli mbiu "Ukuaji wa Makandarasi wa ndani; Fursa na changamoto" na kusisitiza kuwa Makandarasi hao wana wajibu mkubwa katika kuinua uchumi wa nchi na maendeleo ya jamiii.

"Hakikisheni mnazingatia weledi na uzalendo katika shughuli za ukandarasi kwa kutekeleza miradi kwa wakati na kwa viwango vya ubora kulingana na mikataba ili wananchi waweze kupata huduma bora kwa wakati na thamani ya fedha iliyokusudiwa",



*Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega (Mb.) akikabidhi cheti cha ushiriki wa maonesho ya Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2025 kwa Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria za Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi. Bi. Sayi alipokea cheti hicho kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando wakati wa maonesho hayo yaliyofanyika mwezi Mei Jijini Dar es Salaam.*

amesisitiza Mhe. Ulega.

Waziri Ulega amezungumzia umuhimu wa wakandarasi kufanya kazi kwa weledi na kuwapongeza baadhi ya wakandarasi wa ndani kwa kufanyakazi kwa uzalendo na hivyo kumaliza miradi kwa wakati.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya CRB, Mhandisi Farida Mawenya ametoa wito kwa Wakandarasi nchini kuepukana vitendo vya rushwa na kuwataka kushindana kwa haki ili kukuza sekta ya ukandarasi na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi ni jukwaa linalounganisha wadau wa Sekta hiyo kutoka Serikalini na Sekta Binafsi wakiwemo waajiri, makandarasi, wataalam washauri na wengineo kukutana kwa ajili ya kupeana taarifa, kushauriana, kujitathimini na kuweka mikakati madhubuti kwa ajili ya kuboresha ufanisi katika shughuli za ujenzi hapa nchini.



*Mmoja kati ya wakandarasi waliotembelea banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) akisaini kitabu cha wageni katika banda la Mamlaka hiyo wakati wa maonesho ya Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi mwezi Mei, 2025 Jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega (Mb.) akizungumza na watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda la Mamlaka hiyo wakati wa maonesho ya Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi mwezi Mei, 2025 Jijini Dar es Salaam.*




*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akiongea na wazabuni na wadau wa ununuzi wa Umma kutoka taasisi za Serikali wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu matumizi ya Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo (NeST). Mafunzo hayo yamefanyika Mwezi Aprili, 2025 Jijini Mbeya kwa mikoa ya Nyanda za Juu kusini.*

# Wazabuni Nyanda za Juu Kusini wanolewa matumizi ya moduli

**Katika jitihada za kukabili changamoto za ununuzi wa Umma, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeendelea na zoezi la kuwajengea uwezo wazabuni juu ya matumizi ya Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo (NeST).**

Akifungua mafunzo ya siku mbili (tarehe 29 – 30 Aprili, 2025) kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa Umma kutoka taasisi za Serikali kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika jijini Mbeya, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amewataka wadau wa ununuzi wa umma kujifunza kuhusu moduli hiyo vizuri ili kuwawezesha kuisaidia Serikali kupata thamani halisi ya fedha.

"Ili kuendana na matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 pamoja na Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za mwaka 2025, PPAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imetengeneza Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST)," alisema Bw. Sando

Bw. Sando aliongeza kuwa, moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki inafaida nyingi kwa wazabuni, taasisi nunuzi na PPAA kwa kuwa inarahisisha zoezi la uwasilishaji na ushughulikiwaji wa malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

"Moduli hii ina faida mbalimbali zikiwemo, mzabuni kutolazimika kufika katika ofisi za taasisi nunuzi au za PPAA ili kuwasilisha lalamiko au rufaa yake, kupunguza gharama na muda kwa wazabuni wakati wa kuwasilisha malalamiko au rufaa pamoja na kuongeza uwazi katika mchakato wa ushughulikiwaji wa malalamiko na rufaa," aliongeza Bw. Sando

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando aliongeza kuwa hadi kufikia mwezi Aprili 2025, PPAA imeweza kushughulikia mashauri 185 yaliyotokana na michakato mbalimbali ya Ununuzi wa Umma. Aidha, katika mashauri hayo, PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa zabuni 36 wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika. Hatua hii iliepusha Serikali kuingia katika mikataba ambayo ingepelekea kuwa na utekelezaji wa miradi usioridhisha hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma na kuchelewesha maendeleo stahiki kwa wananchi.

Kwa upande wake, Kaminishna Msaidizi Idara ya Sera ya Ununuzi na Ugavi, Wizara ya Fedha, Bi. Emma Komba aliwahimiza washiriki kutumia fursa ya mafunzo hayo kujifunza namna ya uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa kwa njia ya kieletroniki kupitia moduli hiyo ili kuweza kuleta tija katika ununuzi wa umma.

Mafunzo kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa Umma kutoka taasisi za Serikali kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ni muendelezo wa mafunzo yaliyofanyika katika Kanda ya Pwani iliyojumuisha washiriki kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro; Kanda ya Ziwa iliyojumuisha washiriki kutoka mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita, Shinyanga, Mara na Kagera pamoja na Kanda ya Kaskazini iliyojumuisha washiriki kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara.

Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini iliyopatiwa mafunzo kwa siku mbili (Aprili 29 – 30, 2025) ni Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa na Rukwa.




*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando (aliyekaa Katikati, Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Huduma za Sheria PPAA, Bi. Florida Mapunda (aliyekaa kushoto) na Kaminishna Msaidizi Idaraya Sera ya Ununuzi na Ugavi, Wizara ya Fedha, Bi. Emma Komba (alkiyekaa kulia)katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa mafunzo ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo wa NeST kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini jijini Mbeya.*

# Wadau wa ununuzi waaswa kuzingatia maadili kazini

**Wadau wa Ununuzi waaswa kuzingatia maadili na elimu katika Ununuzi wa Umma ili kuiwezesha Serikali kupata thamani halisi ya fedha.**

Wito huo umetolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando alipokuwa akifunga mafunzo ya siku mbili kuhusu matumizi ya Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo (NeST) kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa Umma kutoka taasisi za Serikali kwa Kanda ya Kaskazini yaliyofanyika jijini Arusha.

Bw. Sando amesema kuwa baadhi ya kesi zinazowasilishwa PPAA kwa asilimia kubwa zinakuwa zimesababishwa na ukiukwaji wa maadili.

"Kama wadau katika sekta ya ununuzi wa umma ni muhimu sana kuzingatia maadili kwa sababu ndiyo itakayoipatia serikali thamani halisi ya fedha na heshima, sote tunajua mifumo ya ununuzi ipo lakini inaongozwa na binadamu kama hawana maadili mifumo haina maana," alisema Bw. Sando

Bw. Sando aliongeza kuwa unaweza kutengeneza sheria nzuri sana lakini kama watu hawataamua kuwa watiifu wa sheria hiyo kutakuwa na uvuinjifu mkubwa wa sheria katika nchini hiyo.

"......vivyo hivyo hata sisi tukikosa maadili katika sekta ya ununuzi wa umma tutakuwa na kesi nyingi sana......kutakuwa na upotevu wa fedha za umma," aliongeza Bw. Sando

Kadhalika, Bw. Sando amewataka washiriki walipota fursa ya kuhudhuria mfunzo hayo kwa Kanda ya Kaskazini kuwaelimisha wadau wengine kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST).

Kwa upande wake Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Huduma za Sheria PPAA, Bi. Florida Mapunda amesema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuwaelimisha wadau wa ununuzi wa umma kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo wa NeST katika Kanda ya Kaskazini.



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akifungua mafunzo ya siku mbili (tarehe 10 – 11 Aprili, 2025) kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa Umma kutoka taasisi za Serikali (hawapo pichani) kwa Kanda ya Kaskazini jijini Arusha.*



*Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Huduma za Sheria PPAA, Bi. Florida Mapunda akiwasilisha mada kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo wa NeST kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa Umma kutoka taasisi za Serikali kwa Kanda ya Kaskazini mwezi Aprili, 2025 jijini Arusha.*

"Mtakumbuka kwa sasa Sheria ya Ununuzi wa Umma imeweka takwa la ulazima wa ununuzi wa umma kufanyika kwa njia ya Kieletroniki kupitia mfumo wa NeST. Kutokana na takwa hilo, PPAA imejenga moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko katika mfumo wa NeST ili kuwasaidia wadau wa ununuzi kuwasilisha malalamiko na rufaa kieletroniki pia," amesema Bi. Mapunda.

Bi. Mapunda aliongeza kuwa, moduli imerahisisha zoezi la uwasilishaji wa malalamiko yatokanayo na michakato ya ununuzi wa umma pamoja na kusaidia utunzaji wa kumbukumbu za taarifa za malalamiko na rufaa ambazo zitakuwa zinawasilishwa katika michakato yote ya ununuzi wa umma.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya usambazaji wa vifaa mbalimbali kutoka Karatu 'Gratian General Supplies' Bi. Hilaria Joseph ameipongeza PPAA kwa kuandaa semina hiyo kwani imewasaidia kujua njia ya kuwasilisha malalamiko kwa wakati kupitia kwenye moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo wa NeST.

Mafunzo hayo ya siku mbili kwa Kanda ya Kaskazini yamefanyika jijini Arusha kuanzia tarehe 10 – 11 Aprili, 2025 yanajumuisha mikioa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga.

Awamu ya kwanza ya mafunzo kikanda yalifanyika Kanda ya Ziwa kwa siku tatu ambapo yalijumuisha washiriki zaidi ya 580 mkoani Mwanza kuanzia tarehe 4 – 6 Februari, 2025 yakijumuisha mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Simiyu na Shinyanga.

# PPAA yatoa somo kwa wakandarasi matumizi ya moduli




Baadhi ya wakandarasi na wazabuni wakipatiwa elimu kuhusu moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) katika mfumo wa NeST walipotembela banda la PPAA wakati wa maonesho ya Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi mwezi Mei, 2025 Jijini Dar es Salaam.

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya ununuzi wa umma kwa siku ya pili ya maonesho ya Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2025 yaliyomalizia tarehe 16 Mei 2025, Jijini Dar es Salaam.**

PPAA imetumia maonesho hayo yaliyoratibiwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) kutoa elimu ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) katika mfumo wa NeST kwa wakandarasi, wawakilishi wa serikali, wataalam wa sekta ya ujenzi, pamoja na washiriki wa maonyesho ya kibiashara kwa lengo la kuimarisha sekta za ununuzi wa umma na ujenzi nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando, Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi amesema lengo la PPAA kushiriki katika maonesho hayo ni kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi wa umma kuhusu matumizi sahihi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kieletroniki katika mfumo wa NeST.

"Wakandarasi ni wadau muhimu katika sekta ya ununuzi wa umma hivyo PPAA imeona ni vyema kutumia fursa ya mkutano huu kutoa elimu ya matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa ili iwasaidie kuokoa muda na gharama pamoja na kuisaidia serikali kutekeleza miradi yake kwa wakati uliokusudiwa," amesema Bi. Sayi.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Balozi Aisha Amour, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Mhandisi Mohamed Besta, amewataka Makandarasi nchini kuwa waadilifu na kuzingatia weledi na maadili katika kutekeleza miradi ili kuhakikisha miradi inakamilika kwa thamani ya fedha iliyopangwa.

Mhandisi Besta ametoa wito huo mwezi Mei 2025 Jijini Dar es Salaam wakati wa Kufunga Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2025.

"Napenda kuwakumbusha kuwa kupitia Mkutano huu ndugu zangu Makandarasi kuwa waadilifu na kuzingatia maadili katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa lengo la kuhakikisha thamani halisi ya pesa (value for money) inapatikana kwa kila mradi unaotekelezwa.", amesema Mhandisi Besta.

Kwa upande wake Makamu mwenyekiti wa Bodi ya CRB, Mhandisi Farida Mawenya, ameitaka Mamlaka ya Udhibiti ya Ununuzi wa Umma (PPRA) kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kanuni za upendeleo maalumu kwa wakandarasi wazawa unazingatiwa kikamilifu ili kuwawezesha kushiriki kwa ufanisi katika miradi ya ujenzi nchini.

"Tumefikia maazimio muhimu yatakayoboresha mazingira ya kazi kwa wakandarasi wetu. PPRA ihakikishe inasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa upendeleo maalumu kwa wakandarasi wazawa kama ilivyoainishwa kwenye sheria ya ununuzi wa umma," alisema Mhandisi. Mawenya.

Mkutano huo wa siku mbili tarehe 15 – 16 Mei, 2025 umefanyika na kuwakutanisha wadau mbalimbali takriban 800 wakiwemo wakandarasi, wawakilishi wa serikali, wataalam wa sekta ya ujenzi, pamoja na washiriki wa maonyesho ya kibiashara na kutoa mapendekezo chanya yatakayosaidia kuimarisha sekta ya ujenzi nchini.




Mmoja kati ya wakandarasi akioneshwa jinsi moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) inavyofanya kazi katika mfumo wa NeST alipotembelea banda la maonesho la PPAA mwezi Mei, 2025 Jijini Dar es Salaam.

# PPAA wapewa mbinu za kukabiliana na rushwa kazini



*Mwezeshaji wa mafunzo kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Bw. John Shija akiendelea na zoezi la mafunzo ya kukabiliana na rushwa mahali pa kazi kwa watumishi wa PPAA katika Ofisi za Mamlaka hiyo mwezi Mei, 2025 Jijini Dodoma.*

**Watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wamepatiwa mafunzo ya kukabiliana na rushwa mahali pa kazi ili kudumisha na kuimarisha misingi ya haki na utawala bora mahali pa kazi.**

Akifungua mafunzo hayo katika Ofisi za PPAA Jijini Dodoma kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma, Bw. James Sando, Meneja wa Huduma za Sheria wa PPAA, Bi. Florida Mapunda amewasihi watumishi wa Mamlaka ya Rufani kutumia mafunzo hayo kama chachu ya kukabiliana na rushwa mahali pa kazi na kuimarisha misingi ya haki na utawala bora katika utendaji kazi wa kila siku.

"Mapambano dhidi ya rushwa mahali kazini ni muhimu kwani yanasaidia kuongeza ufanisi katika utendaji, lakini pia huwafanya watumishi kuwa salama zaidi katika utendaji kazi wa kila siku," amesema Bi. Mapunda

Bi. Mapunda amewaasa watumishi wa PPAA kuhakikisha kuwa wanakuwa waadilifu na kuzingatia kanuni za maadili ya utumishi wa umma za Mwaka 2005. "PPAA ni taasisi inayojihusisha na masuala ya haki, hivyo sisi kama watumishi tunaosimamia haki ni muhimu kusimamia haki kwa maendeleo na maslahi ya taifa kwa ujumla," amesema Bi. Mapunda

Kwa upande wake mwezeshaji wa mafunzo hayo kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Bw. John Shija, amesema kuwa mafanikio ya kuzuia rushwa ni pamoja na kuongeza nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma, wafanyabiashara na watoa huduma mbalimbali.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Shija amesema kuwa mkakati wa kupambana rushwa nchini NACS umetiliwa mkazo zaidi katika kuzuia rushwa kupitia utawala bora, uwazi, usimamizi wa uadilifu na uwajibikaji katika jamii, na kugundua mapema vitendo vya rushwa vinavyoweza kujitokeza ili kuongeza hatua tendaji zinazotekelezwa na vyombo vya sheria.

"Tumekutana hapa kwa lengo la kujifunza na kukumbushana masuala ya uwajibikaji kwetu sisi watumishi wa umma, hivyo tupende kujifunza vitu vipya hususan mikakati ya kukabilina na rushwa mahali pa kazi na katika jamii kwa ujumla," amesema Bw. Shija na kuongeza kuwa ni vyema kila mtumishi kujiepuka na vitendo vya rushwa na kuzingatia maadili wakati wanapotoa huduma kwa umma.

Mada zilizowasilishwa wakati wa mafunzo hayo ni pamoja na mikakati ya kuzuia rushwa, utawala bora, pamoja na nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma mahali pa kazi.



*Meneja wa Huduma za Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Florida Mapunda akizungumza na watumishi wa PPAA wakati akifungua mafunzo ya kukabiliana na rushwa mahali pa kazi katika Ofisi za Mamlaka hiyo mwezi Mei, 2025 Jijini Dodoma.*



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akifungua mafunzo ya siku moja kwa wazabuni wa mkoa wa Dodoma na mikoa Jirani (hawapo pichani) mwezi Juni, 2025 jijini Dodoma.*

# Wazabuni wa Dodoma wapigwa msasa matumizi ya moduli

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wazabuni kuhusu matumizi ya Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo (NeST).**

Akifungua mafunzo ya siku moja tarehe 18 Juni, 2025 kwa wazabuni wa Mkoa wa Dodoma na mikoa Jirani, Jijini Dodoma, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amewaasa kujifunza matumizi ya moduli hiyo ili waweze kuitumia wakati wa kuwasilisha malalamiko na rufaa zitokanazo na michakato ya zabuni.

Bw. Sando amesema kuwa moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST inafaida kwa wazabuni, taasisi nunuzi na PPAA ikiwemo kuokoa muda, gharama na kuongeza uwazi na uwajibikaji. “Moduli hii ina okoa muda na gharama kwa mzabuni kwa kuwa hatalazimika kusafiri ili aweze kuwasilisha malalamiko au rufaa yake PPAA,” alisema Bw. Sando

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando amesema PPAA imeweza kushughulikia mashauri 177 yaliyotokana na michakato mbalimbali ya Ununuzi wa Umma, ambapo katika mashauri hayo, PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa zabuni 37 kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika, kwa kufanya hivyo PPAA iliisadia Serikali kupata thamani halisi ya fedha katika miradi hiyo.

Kwa upande wa wazabuni walioshiriki mafunzo hayo wakiongozwa na Mhandisi Beda Labule, amesema kuwa utaratibu wa kuwasilisha rufaa kieletroniki umerahisisha zoezi la kuwasilisha malalamiko na kukata rufaa kwa wazabuni ambao hawataridhika na sababu za kuondolewa kwao ikilinganishwa na ilivyokuwa awali.

“Kama mtakumbuka awali mzabuni mwenye malalamiko au rufaa alipaswa kusafiri kwenda katika Ofisi za PPAA kuwasilisha rufaa yake, ila sasa baada ya Serikali kuweka Moduli hii ya kupokea na kushughulikia malalamiko imeturahisisha zoezi la kuwasilisha malalamiko yetu PPAA,” amesema Mhandisi Labule

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Jofenai Investment, Bi. Jofenai-joy Felician amesema moduli imerahisisha zoezi la uwasilishaji wa malalamiko yatokanayo na michakato ya ununuzi wa umma pamoja na kusaidia kuokoa gharama na muda pamoja na kuongeza uwazi.

“Mimi kama mzabuni nimewahi kupatwa na changamoto mbalimbali wakati wa uwasilishaji wa rufaa kwa wakati, ni imani yangu kupitia moduli hii itasaidia pia utunzaji wa kumbukumbu za taarifa za rufaa ambazo zitakuwa zinawasilishwa katika michakato yote ya ununuzi wa umma,” amesema Bi. Felician

Mafunzo hayo ya siku moja kwa wazabuni wa Mkoa wa Dodoma na mikoa Jirani yanafuatia mafunzo ya awamu ya kwanza yaliyofanyika Kanda ya Ziwa tarehe 4 – 6 Februari, 2025 yalijumuisha mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Simiyu na Shinyanga.

Aidha, awamu ya pili ya mafunzo yalifanyika Kanda ya Kaskazini tarehe 10 Aprili, 2025 yakijumuisha mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Kadhalika, mafunzo ya awamu ya Tatu yalifanyika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini tarehe 29 na 30, 2025 ambapo yalijumuisha mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa.



*Sehemu ya wazabuni/washiriki wa mafunzo ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST kutoka mkoa wa Dodoma na mikoa Jirani mwezi Juni, 2025 jijini Dodoma.*

# Zingatieni maadili ya kazi, Sando awaasa wadau wa ununuzi



**Wadau wa ununuzi wameaswa kuzingatia maadili na elimu katika ununuzi wa umma ili kuiwezesha Serikali kupata thamani halisi ya fedha.**

Wito huo umetolewa na Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando alipokuwa akifunga mafunzo ya siku mbili kuhusu matumizi ya Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo (NeST) kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa Umma kutoka taasisi za Serikali kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika jijini Mbeya.

"Kama wadau katika sekta ya ununuzi wa umma ni muhimu sana kuzingatia maadili kwa sababu ndiyo itakayoipatia serikali thamani halisi ya fedha na heshima, sote tunajua mifumo ya ununuzi ipo lakini inaongozwa na binadamu kama hawana maadili mifumo haina maana," amesema Bw. Sando

Bw. Sando aliongeza kuwa Serikali inaweza kutengeneza sheria nzuri sana lakini kama watu hawataamua kuwa watiifu wa sheria hiyo kutakuwa na uvuinjifu mkubwa wa sheria katika nchini hiyo."......vivyo hivyo hata sisi tukikosa maadili katika sekta ya ununuzi wa umma tutakuwa na kesi nyingi sana......kutakuwa na upotevu wa fedha za umma," ameongeza Bw. Sando

Kadhalika, Bw. Sando amewataka washiriki walipota fursa ya kuhudhuria mfunzo hayo kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuwaelimisha wadau wengine kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST).


Naye mmoja wa wazabuni kutoka Wilayani Chunya, Bi. Lightnes Mkemi ameipongeza PPAA kwa kuandaa mafunzo hayo na kuiomba Mamlaka hiyo kuendelea kutoa mafunzo hayo katika ngazi za wilaya ili kuwasaidia wazabuni wengi zaidi kufahamu namna ya kuwasilisha malalamiko na rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi kwa wakati kupitia moduli iliyopo katika mfumo wa NeST.

Kadhalika, Mhandisi Deogratius Ndamugoba ameishukuru PPAA kwa kuanzisha moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo (NeST) kwani moduli hiyo itawarahisishia utaratibu wa kuwasilisha malalamiko na rufaa pindi ambapo hawataridhishwa na michakato ya ununuzi wa umma.

Mafunzo hayo ya siku mbili kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yamefanyika jijini Mbeya kuanzia tarehe 29 – 30 Aprili, 2025 yalihudhuriwa na washiriki 240 kutoka mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, na Rukwa.

Awamu ya kwanza ya mafunzo kikanda yalifanyika Kanda ya Ziwa kwa siku tatu ambapo yalijumuisha washiriki zaidi ya 580 mkoani Mwanza kuanzia tarehe 4 – 6 Februari, 2025 yakijumuisha mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Simiyu na Shinyanga.

Awamu ya Pili ya mafunzo yalifanyika Kanda ya Kaskazini yakijumuisha washiriki takriban 240 kutoka mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga yalifanyika tarehe 10 – 11 Aprili, 2025 jijini Arusha.



# Rufaa dhidi ya Chuo Kikuu Mzumbe yakwaa kigingi

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imetupa shauri la zabuni dhidi ya Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa kufunguliwa nje ya muda uliopangwa kisheria.**

Rufaa hiyo iliwasilishwa na Kampuni ya Mtatiro Auto Engineers and Decorators kuhusu zabuni ya ununuzi wa gari.

Mlalamikaji alidai baada ya kuarifiwa zabuni yake ilienguliwa kwa kuwa haikuwa na bei nafuu zaidi kwenye hatua ya tathmini ya kifedha, hakukubaliana na sababu iliyotolewa.

Hivyo tarehe 31 Disemba 2024 aliwasilisha malalamiko yake kwa Afisa Masuuli wa Chuo Kikuu cha Mzumbe. Baada ya kutopatiwa majibu ndani ya siku tano za kazi tarehe 22 Januari 2025 aliwasilisha rufaa mbele ya PPAA.

Baada ya kupokea rufaa, PPAA ilimfahamisha mlalamikiwa kuhusu rufaa hiyo na ikamuelekeza kuwasilisha majibu. Chuo Kikuu cha Mzumbe kilithibitisha msimamo wake kwamba mlalamikaji alienguliwa katika mchakato wa zabuni husika kwa njia ya haki.

Aidha, mlalamikiwa aliwasilisha pingamizi la awali (PO) likilenga kuona kama rufaa iliyowasilishwa PPAA kwa njia sahihi; lakini pia PPAA ililenga kujibu hoja zifuatazo: kama zabuni ya mlalamikaji ilienguliwa kihalali; na ni nafuu gani kama ipo, wanazostahili pande zote?

Mlalamikiwa alidai rufaa imewasilishwa mapema PPAA kinyume na matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, kwani sheria inamtaka mlalamikaji kuwasilisha malalamiko yake kwa Afisa Masuuli kabla ya kuwasilisha rufaa PPAA.

Chuo Kikuu cha Mzumbe kilisisitiza kwamba, kama mlalamikaji hakuridhika na kuenguliwa kwake, alipaswa kuwasilisha malalamiko yake kwa Afisa Masuuli ndani ya siku tano za kazi tangu alipopokea taarifa ya kusudio la kutoa zabuni. Kinyume chake, mlalamikaji aliwasilisha rufaa moja kwa moja PPAA, hivyo kusababisha rufaa kuwasilishwa mapema kabla ya kukidhi hatua nyingine za kisheria.

Aidha, Chuo Kikuu cha Mzumbe kilifafanua kwamba hata kama ingewezekana kudhani kwamba mlalamikaji aliwasilisha malalamiko yake kwa Afisa Masuuli kwa njia sahihi, rufaa kwa PPAA iliwasilishwa nje ya muda, kinyume na matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Chuo Kikuu cha Mzumbe kilisisitiza kwamba kifungu hicho kinampa mlalamikaji haki ya kuleta rufaa moja kwa moja PPAA ndani ya siku tano za kazi ikiwa Afisa Masuuli ameshindwa kutoa uamuzi wake ndani ya muda ulioainishwa kisheria.

Mlalamikiwa aliongeza kusema ikiwa malalamiko yaliwasilishwa tarehe 31 Desemba 2024, endapo siku zitahesabika kuanzia tarehe ambayo mlalamikiwa alipaswa kutoa uamuzi wake tarehe 8 Januari 2025, baada ya hapo mlalamikaji alipaswa kuwasilisha rufaa yake kabla ya tarehe 15 Januari 2025, badala yake rufaa iliwasilishwa tarehe 22 Januari 2025.

Hivyo, rufaa iliwasilishwa nje ya muda uliainishwa kisheria. Hivyo Chuo Kikuu Mzumbe kiliomba Mamlaka ya Rufani kutupilia mbali rufaa husika kwa kuwasilishwa kinyume cha matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Kwa upande wake, Kampuni ya Mtatiro Auto Engineers and Decorators ilieleza rufaa haikuwasilishwa mapema PPAA kama ilivyodaiwa na mlalamikiwa.

Mlalamikaji alidai aliwasilisha malalamiko yake kwa Afisa Masuuli wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kabla ya kuwasilisha Rufaa mbele ya Mamlaka ya Rufani. Mlalamikaji alisema kwamba malalamiko yake yaliwasilishwa kwa Afisa Masuuli tarehe 4 Januari 2025 kwa njia ya barua pepe ya william. mwegoha@muya .ac.tz.



Hata hivyo, mlalamikaji baada ya kuhesabiwa siku kwa mujibu wa sheria, alikubali kwamba rufaa iliwasilishwa nje ya muda. Aidha, mlalamikaji aliiomba PPAA kutoa upendeleo maalumu kutokana na sababu kwamba malalamiko yake yaliwasilishwa ndani ya muda. Hivyo, PPAA inapaswa kuendelea kusikiliza rufaa hiyo kwa kuzingatia misingi ya sheria.

Mlalamikiwa alijibu kuwa barua pepe iliyotumiwa na mlalamikaji kuwasilisha malalamiko yake ni ya mtu binafsi hivyo mlalamikiwa hakuwa na wajibu wa kujibu malalamiko yaliyowasilishwa. Barua pepe rasmi ya kupokea malalamiko imeainishwa kwenye mfumo wa NeST ambayo ni mu@ mzumbe.ac.tz.

Ili kubaini misingi ya rufaa, PPAA ilipitia rufaa hiyo na kubaini sheria inaonesha wazi kuwa ikiwa mlalamikaji hakuridhika na uamuzi wa Taasisi Nunuzi, anapaswa kuwasilisha malalamiko yake kwa Taasisi Nunuzi ndani ya siku tano za kazi tangu alipofahamu jambo analolilalamikia.

Taasisi Nunuzi inapaswa kutoa uamuzi wake ndani ya siku tano za kazi, na kama haitafanya hivyo, mlalamikaji anapaswa kuwasilisha rufaa yake PPAA ndani ya siku tano za kazi.

PPAA ilibaini Chuo Kikuu cha Mzumbe kilipaswa kutoa uamuzi wake kufikia tarehe 10 Januari 2025. Hata hivyo, hakikutoa uamuzi ndani ya muda ulioainishwa kisheria.

Baada ya kushindwa kupata uamuzi ndani ya siku tano za kazi mlalamikaji alipaswa kuwasilisha rufaa yake ndani ya siku tano za kazi ambazo ziliishia tarehe 17 Januari 2025. Badala yake mlalamikaji aliwasilisha rufaa hiyo tarehe 22 Januari 2025, nje ya muda ulioainishwa kisheria.

Aidha, PPAA baada ya kupitia hoja za pande zote mbili na matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ilibaini rufaa iliwasilishwa nje ya muda ulioainishwa kisheria. Hivyo PPAA iliitupilia mbali rufaa ya mlalamikaji kwa kuwasilishwa kinyume cha matakwa ya sheria.




# PPAA yatoa elimu matumizi ya moduli Wiki ya Utumishi wa Umma

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeshiriki maadhimisho ya kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma, yanayojumuisha Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Taasisi mbalimbali za Umma kwa lengo la kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi nchini na wananchi kwa ujumla.**

PPAA imeshiriki maadhimisho hayo yaliyoratibiwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma kwa lengo la kutoa elimu pamoja na kuonesha uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Mamlaka ya Rufani.

Akiongea kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma PPAA, Bw. Nelson Kessy amesema kupitia maadhimisho ya Wiki ya Utumishi, PPAA imepata fursa ya kutoa elimu kuhusu matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST.

"Pamoja na mambo mengine, moduli hii imesaidia kuokoa muda, gharama, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma na kutunza kumbukumbu kwa ujumla," amesema Bw. Kessy

Bw. Kessy ameongeza kuwa PPAA imetumia jitihada mbalimbali za kuwapatia wazabuni mafunzo mahususi kuhusu matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST inawafikia wadau wa ununuzi wa umma ili kuisaidia Serikali kupata thamani halisi ya fedha.

Moja ya jitihada hizo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma katika Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati. Aidha, katika mafunzo hayo PPAA ilifanikiwa kutoa elimu kwa wazabuni 873 na wakuu wa Idara/ Vitengo vya ununuzi na sheria wapatao 1,588 kutoka katika taasisi nunuzi 500.

Sanjari na mafunzo, PPAA imetumia maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kuelimisha wananchi na wadau wa ununuzi kuhusu matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia Malalamiko na rufaa kieletroniki ikiwemo kuokoa muda na gharama.

Maadhimisho ya wiki ya Utumishi ya mwaka 2025 yamezikutanisha pamoja Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Taasisi mbalimbali za Umma, kwa lengo la kuonesha uwajibikaji wa taasisi hizo katika utoaji wa huduma na bidhaa kwa wananchi pamoja na kutoa elimu kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi hizo.

Awali akifungua rasmi maadhimisho ya Wiki ya Utumishi, Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb.) alizisisitiza taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa zinatoa kipaumbele kikubwa katika matumizi ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma.

"Napenda kutoa wito kwa taasisi za umma zote kuhakikisha zinatumia TEHAMA vizuri ili wananchi waweze kuendelea kupata huduma bora haraka na kwa urahisi," alisema Waziri Simbachawene.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo kitaifa ni: "Himiza Matumizi ya Mifumo ya Kidigiti ili kuongeza Upatikanaji wa Taarifa na kuchagiza Uwajibikaji".

Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika huadhimishwa kila mwaka tarehe 23 Juni na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU), ikiwa ni ishara ya kutambua mchango muhimu wa watumishi wa umma katika maendeleo ya nchi zao na bara kwa ujumla.



# HABARIPICHA




*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb.) akiongea na watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wakati alipotembelea banda la Mamlaka hiyo kabla ya kuzindua rasmi Kongamano la Tisa la Ununuzi wa Umma lililofanyika mwezi Juni, 2025 Jijini Arusha.*




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb.) akizungumza na watumishi wa PPAA alipotembelea Banda la PPAA katika maonesho ya Kongamano la Tisa la Ununuzi mwezi Juni, 2025 Jijini Arusha.*



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akizungumza na Mwandishi wa Habari wa TBC1 aliposhiriki Kipindi cha JamboTanzania kilichokuwa na mada iliyohusu mchango wa Tehama katika ununuzi wa umma nchini mwezi Aprili 2025, Jijini Dodoma.*

# HABARIPICHA




*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando (aliyekaa Katikati, Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Huduma za Sheria PPAA, Bi. Florida Mapunda (aliyekaa kushoto) na Kaminishna Msaidizi Idaraya Sera ya Ununuzi na Ugavi, Wizara ya Fedha, Bi. Emma Komba (alkiyekaa kulia) katika picha ya pamoja na baadhi ya watumishi wa PPAA baada ya kukamilika kwa mafunzo ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika mfumo wa NeST kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini mwezi Aprili 2025 jijini Mbeya.*



*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb.) akikabidhi zawadi ya cheti cha udhamini wa Kongamano la tisa la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2025 kwa Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando mwezi Juni, 2025 jijini Arusha. Wengine pichani ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba (pembeni mwa Katibu Mtendaji wa PPAA) na Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi wa PPRA, Dkt. Leonada Mwagike.*




*Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Mhe. Jaji (Mstaafu) Awadh Bawazir (aliyekaa katikati) katika picha ya pamoja na wajumbe wa Mamlaka ya Rufani na baadhi ya watumishi wa PPAA katika Ofisi za Mamlaka hiyo mwezi Aprili, 2025 Jijini Dodoma.*